United Nations

A/HRC/60/35/Add.4

General Assembly

Distr.: General
8 December 2025

Original: English

Baraza la Haki za Binadamu
Kikao cha sitini
Septemba 8–Oktoba 3, 2025
Kipengele cha ajenda 3
Kukuza na kulinda haki zote za binadamu, haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni, ikiwa ni pamoja na haki ya maendeleo

Kutoweka kwa lazima katika muktadha wa ulinzi wa ardhi, maliasili na mazingira

Ripoti ya Jopokazi kuhusu Kutoweka kwa Kulazimishwa au Kutokusudiwa

Muhtasari

Katika ripoti hii, Jopokazi ya Kutoweka kwa Kulazimishwa au Kutokusudiwa linachunguza mwenendo wa kutisha wa kimataifa wa kutoweka kwa lazima kunaowalenga watu wanaotetea ardhi, maliasili, na mazingira (watetezi wa LNRE). Kutoweka huku mara nyingi hutokea katika muktadha wa ubaguzi wa kimfumo, utawala dhaifu wa sheria, na maslahi yenye nguvu ya kiuchumi, pamoja na ushiriki au idhini ya mamlaka za Serikali. Ripoti hii inaangazia athari kwa Jamii Asilia, Jamii walio na Asili ya Kiafrika, na idadi ya watu wa vijijini, na inasisitiza jukumu la makampuni ya biashara na taasisi za fedha katika kuwezesha au kutekeleza ukiukwaji huo kupitia kukubali kwa Serikali.

Ripoti inatoa uchambuzi kamili wa sababu za hatari, mifumo ya kutokujali, na vichocheo vya kimuundo vinavyosababisha kutoweka kwa lazima. Ripoti hii pia inaelezea majukumu ya watendaji wa Serikali na wasio wa Serikali chini ya sheria ya kimataifa, na inatoa mapendekezo thabiti ili kuhakikisha kuzuia, uwajibikaji, na fidia kamili kwa waathiriwa na jamii zilizoathiriwa.

I. Utangulizi

1. Wakati wa kikao cha 131, Jopokazi la Kutoweka kwa Watu kwa Lazima au Kutoweka Kusiokusudiwa (“Jopokazi”) liliamua kufanya utafiti wa kina juu ya kutoweka kuliotekelezwa kwenye muktadha wa ulinzi wa ardhi, maliasili, na mazingira)[1]. Kwa lengo hili, Jopokazi lilifanya mashauriano kadhaa[2], ikiwa ni pamoja na mashauriano kwenye kanda za Amerika, Asia na Afrika, na takriban mahojiano hamsini na wamiliki wa Taratibu Maalum za Umoja wa Mataifa. na maafisa wa haki za binadamu wa Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu (OHCHR). Jopokazi lilipokea jumla ya mawasilisho thelathini na moja kwa wito wake wa maoni ya maandishi, yakiwemo mawili kutoka Nchi Wanachama, moja kutoka OHCHR, moja kutoka taasisi ya kitaifa, mchango mmoja wa mtu binafsi, na mawasilisho 25 ya pamoja yanayowakilisha asasi za kiraia na wasomi 264[3]. Jopokazi lingependa kutoa shukrani zake za dhati kwa wale walioshiriki katika mashauriano na mahojiano yake na wale waliowasilisha majibu kwa maandishi.

2. Katika miaka ya hivi karibuni, kumeibuka mwelekeo unaotia wasiwasi na uliorekodiwa[4] ambapo watetezi wa ardhi, maliasili, na mazingira (watetezi wa LNRE) wamezidi kutoweka kwa lazima kwa sababu ya utetezi wao. Watetezi hawa mara nyingi wanakabiliwa na hatari kubwa zinazotokana na; maeneo ya mbali ambayo wanafanyia kazi, maslahi ya kiuchumi wanayoyapinga, au kuwa wao ni wa jamii asilia au jamii zilizotengwa.

3. Jopokazi lingependa kutambua kwamba ripoti hii inatumia neno "watetezi wa LNRE" kumaanisha watu binafsi wanaohusika katika ulinzi wa ardhi, maliasili, na mazingira, bila kujali kama wanajitambulisha kama "watetezi". Kupitia neno hili jumuishi, Jopokazi linatafuta kutambua kwa upana watu wanaohusika katika juhudi hizi, ambazo zinajumuisha, jamii za vijijini, na Jamii Asilia wanaopinga unyang'anyi wa ardhi, wakulima wadogo au wavuvi wanaolinda riziki zao, wanasheria wanaopinga leseni na makubaliano ya serikali kwa miradi ya maendeleo, waandishi wa habari wanaochunguza na kufichua uhalifu wa mazingira, na wanaharakati wa vijana wanaharakati wanaohamasisha kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, na juhudi zinginezo..

4. Jopokazi limesisitiza mara kwa mara kutotenganishwa kwa haki za kiuchumi, kijamii, na kitamaduni kutoka kwa haki za kiraia na kisiasa katika muktadha wa kutoweka kwa watu kwa lazima, likizingatia kwamba watetezi wa haki za kiuchumi, kijamii, na kitamaduni mara nyingi huwa wanalengwa sana kutoweshwa kwa lazima, kama njia ya kukandamiza utetezi wao.[5] Uhusiano wa haki hizi unaonekana hasa katika visa vya kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE.

---

[1] A/HRC/WGEID/131/1, para. 19.

[2] Jopokazi linapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa the Berkeley Human Rights Clinic, CEJIL, NOMADESC, ALLIED, Natural Justice, the American Bar Association, na ofisi OHCHR ya Asia ya Kusini-mashariki kwa msaada wao muhimu katika maandalizi, na wakati wa mashauriano ya kikanda. Kundi Kazi pia linatoa shukrani zake kwa Ms. Elisa Morguera, Ms. Mary Lawlor, Ms. Astrid Puentes Riaño, Ms. Fernanda Hopenhaym, Ms. Anexa Alfred, Mr. Michel Forst, Ms. Roxanna Altholz, Ms. Radhika Kapoor, Ms. Viviana Krsticevic from CEJIL, Ms. Alejandra Gonza from Global Rights Advocacy, Ms. Alejandra Ancheita from Proyecto de Derechos Económicos Sociales y Culturales (PRODESC), the University of Nuremberg and the Berkeley Human Rights Clinic kwa mchango wao mkubwa katika utayarishaji wa ripoti hii.

[3] Wito wa michango na michango iliyopokelewa (isipokuwa ile ambayo ni ya siri) unaweza kupatikana hapa:https://www.ohchr.org/en/calls-for-input/2025/call-submissions-thematic-report-enforced-disappearances-context-defense-land. Isipokuwa imeonyeshwa vinginevyo, taarifa zilizomo katika utafiti huu zinategemea mawasilisho yaliyopokelewa na mashauriano yaliyofanyika. Marejeleo ya moja kwa moja kwa mawasilisho, ikiwa si ya siri, yatafanywa tu wakati takwimu zitatolewa au ikiwa ziliombwa waziwazi.

[4] Angalia, Global Witness, “Missing Voices: The violent erasure of land and environmental defenders”, 10 September 2024; Alliance for Land, Indigenous and Environmental Defenders, “Uncovering the Hidden Iceberg: A Global Perspective”, 2024.

[5] A/HRC/30/38/Add.5, paras. 73-75.

5. Ufafanuzi wa kutoweka kwa lazima unahusisha ushiriki wa mawakala wa Serikali, angalau kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kwa kukubali kimya kimya. Kutoweka kunakofanywa na mtendaji asiye wa Serikali kunastahili kuwa kutoweka kwa lazima wakati, kunapotendwa na uungaji mkono wa serikali kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja. Watendaji wasio wa Serikali wanaweza kujumlisha wanamgambo waliojihami wasio wa Serikali, vikundi vya uhalifu, mashirika ya kimataifa na makampuni mengine ya biashara, taasisi za fedha za kimataifa, na makampuni binafsi ya kijeshi na usalama, miongoni mwa mengine. Watendaji wasio wa Serikali wanaofanya kazi kama za serikali au udhibiti halisi juu ya eneo au idadi ya watu, bila idhini, au usaidizi wa Serikali, wanaweza kutenda vitendo sawa na kutoweka kwa lazima.[6]

6. Kuhusu vitendo vinavyofanywa na makampuni ya biashara, Jopokazi linatilia maanani umuhimu wa Kanuni za Mwongozo za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu (UNGP). Hasa, makampuni ya biashara yana jukumu la kuepuka kukiuka haki za binadamu, kama vile haki ya kutotowesha watu kwa lazima, na kushughulikia athari za ushiriki wowote wanaoweza kuwa nao katika ukiukaji huo. Pia, wanatarajiwa kuzuia, kupunguza na kurekebisha athari mbaya za haki za binadamu zinazohusiana moja kwa moja na shughuli zao, bidhaa au huduma, au mahusiano ya kibiashara, hata wakati hawajachangia athari hizo.[7]

7. Kwa mujibu wa mamlaka yake ya kibinadamu, na kwa pamoja na Taratibu zingine Maalum, Jopokazi limepokea mawasiliano kuhusu visa vya kutoweka kwa lazima katika muktadha wa ulinzi wa LNRE katika mataifa kadhaa, ikiwa ni pamoja na Uchina,[8] Colombia,[9] Guatemala,[10] India,[11] Mexiko,[12] Nepal,[13] Nicaragua,[14] Peru,[15] Ufilipino,[16] na Thailand.[17] Jopokazi pia limetuma mawasiliano ya visa vinavyohusiana na kutoweka kwa lazima Argentina,[18] Jamhuri ya Kiislamu ya Iran,[19] Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao,[20] Grand Duchy ya Luxembourg,[21] Urusi,[22] Uganda,[23] na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.[24]

8. Ingawa si mada ya ripoti hii, changamoto hizi zinazidishwa zaidi katika miktadha ya migogoro ya silaha au migogoro ya mipaka, ambayo huongeza kuenea kwa kutoweka kwa watu kwa lazima, ikiwa ni pamoja na watetezi wa LNRE.

[6] A/HRC/42/40, para. 94

[7] Guiding Principles on Business and Human Rights: Implementing the United Nations “Protect, Respect and Remedy” Framework, in particular Guiding Principles 11, 13 and 14. Pia A/HRC/RES/17/4.

[8] A/HRC/WGEID/116/1, para. 37

[9] E/CN.4/2002/79, para. 93, E/CN.4/1989/18, para. 79.

[10] E/CN.4/1994/26, para. 215.

[11] A/HRC/WGEID/118/1, para. 59 na IND 9/2019.

[12] E/CN.4/2004/58, para. 195,E/CN.4/1998/43, para. 261 na MEX 1/2023

[13] E/CN.4/2003/70, para. 127.

[14] A/HRC/WGEID/132/1, para. 83 (a).

[15] E/CW.4/1991/20, para. 299 na E/CN.4/1989/18, para. 226.

[16] A/HRC/WGEID/131/1, para. 99.

[17] A/HRC/WGEID/103/1, para. 174, A/HRC/WGEID/132/1, para. 114 na THA 2/2019.

[18] ARG 1/2023.

[19] IRN 37/2021.

[20] LAO 3/2012.

[21] LUX 1/2023.

[22] RUS 3/2014.

[23] UGA 4/2024

[24] TZA 4/2024 na TZA 3/2025.

II. Hulka na Sababu Hatarishi Zinavyohusiana na Kutoweka kwa Lazima kwa Watetezi wa LNRE

9. Jopokazi limepokea mawasiliano kuhusu kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE—hasa wakiwahusisha Jamii Asilia—tangu miaka ya 1980. Tangu 2016, wataalamu huru wameelezea wasiwasi kuhusu "kiwango cha kushangaza" cha mashambulizi dhidi ya watetezi wa LNRE.[25] Licha ya kuongezeka kwa umakini wa kimataifa, kiwango cha vurugu dhidi ya watetezi wa haki za binadamu kwa ujumla, na dhidi ya wale wanaofanya kazi ya kutetea LNRE haswa, kimekuwa "mgogoro wa kimataifa".[26]Jopokazi linajuta kwamba kuna ukosefu wa data maalum kuhusu kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE. Hata hivyo, data nyingine zinaweza kutoa ufahamu kuhusu kiwango halisi cha hatari ambazo watetezi hawa wanakabiliwa nazo. Kulingana na takwimu zilizopo, kati ya 2012 na 2022, watetezi 1,733 wa LNRE waliuawa—wastani wa mmoja kila baada ya siku mbili.[27] Kwa mfano, mwaka wa 2022, watetezi 177 wa LNRE waliuawa, huku 36% wakiwa Jamii Asilia, hasa kutokana na migogoro inayohusisha kilimo biashara, uchimbaji madini, ukataji miti, na miradi ya miundombinu.[28] Kufikia mwaka wa 2023, idadi ya mauaji ilikuwa imeongezeka hadi 196, huku 43% wakiwa Jamii Asilia na 12% wakiwa wanawake, huku wengine wengi wakikabiliwa na vitisho, vurugu, unyanyapaa, na uhalifu.[29]

10. Kwa mujibu wa mawasiliano yaliyopokelewa na Jopokazi, vurugu nyingi dhidi ya watetezi wa LNRE hufanyika katika nchi zinazoendelea ambazo zinakumbwa na utawala dhaifu wa sheria, ufisadi na ukosefu wa usawa. Mara nyingi, mataifa husika pia hukosa sheria kamili kuhusu mwenendo na majukumu ya haki za binadamu ya makampuni ya biashara. Hakika, kuna mambo mengi ya hatari yanayochangia kutoweka kwa watetezi wa LNRE. Hata hivyo, jambo la kawaida miongoni mwa haya ni tofauti ya madaraka kati ya watetezi hawa na maslahi yenye nguvu wanayoyapinga. Walivyoandika wataalamu wa Umoja wa Mataifa,[30] mashirika ya asasi za kiraia,[31] mashirika na kimataifa,[32] kutoweka kwa watetezi wa LNRE mara nyingi ni matokeo ya ushirikiano kati ya Serikali, makampuni ya biashara, na vikundi vya uhalifu, mara nyingi kukiwa na lengo ya kulinda na kuongeza faida inayotokana na viwanda vya uchimbaji madini, biashara ya kilimo, miradi ya nishati, na miradi ya maendeleo, miongoni mwa mengine.

A. Utambulisho na jamii

11. Mjumbe Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu amewaelezea watetezi wa LNRE kama "mojawapo ya vikundi vya watetezi vyenye tofauti kubwa" vyenye "watu mbalimbali, wasifu na njia mbalimbali ...".[33] Wengi huwa watetezi "kwa bahati mbaya" au "umuhimu", na wanalazimika kuchukua hatua kujibu vitisho dhidi ya mazingira, ardhi yao, au maliasili.[34] Hakika, watetezi wa LNRE wanakabiliwa na hatari

[25] A/71/281, para. 2. Pia A/HRC/26/25.
[26] A/71/281, para. 26.
[27] Global Witness, "Decade of Defiance: Ten Years of Reporting Land and Environmental Activism Worldwide", September 2022, p. 16.
[28] Global Witness, "Standing Firm: The Land and Environmental Defenders on the Frontlines of the Climate Crisis", 2023, p. 11.
[29] Global Witness, "Missing Voices: The violent erasure of land and environmental defenders", 10 September 2024.
[30] Mexico must clarify fate and whereabouts of human rights defenders Ricardo Lagunes and Antonio Díaz and business must collaborate: UN experts, 20 February 2023; Pia, kwa mfano, RUS 3/2014, THA 2/2016, MEX 9/2021, UGA 4/2024, na TZA 1/2024, GBA 4/2024 na USA 10/2024.
[31] Global Witness, "Decade of Defiance: Ten Years of Reporting Land and Environmental Activism Worldwide"; Global Witness, "Standing Firm: The Land and Environmental Defenders on the Frontlines of the Climate Crisis"; Global Witness, "Missing Voices: The violent erasure of land and environmental defenders", 10 September 2024.
[32] UNECE, AC/WGP-24/Inf.16; UNDP, "UNDP reports reveal the human rights defenders are still targeted by businesses, with 37% resulting in violence leading to loss of life.", 11 February 2024.
[33] A/71/281, para. 53.
[34] Ibid.

kubwa kwa sababu wanajipata katikati ya tabaka zenye nguvu zaidi za makampuni, fedha, na serikali duniani, na baadhi ya maliasili zenye thamani kubwa zaidi duniani, ambazo mara nyingi ziko katika maeneo ya jamii zilizo hatarini zaidi.

12. Kimataifa, vsa 1,538 vya ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya watetezi wa haki za binadamu viliripotiwa kutoka nchi 105 mwaka wa 2023, huku wale wanaowatetea Jamii Asilia, Jamii walio na asili ya Kiafrika, na jamii za wakulima wadogo huko bara za Amerika wakiwa walengwa zaidi.[35] Kutambuliwa kama watetezi wa haki za binadamu kunaweza kuwasaidia watetezi wa LNRE kupata mifumo ya ulinzi, kuongeza mwonekano, na kupunguza hatari ya kutoweka kwa lazima. Hata hivyo, wengi hawatambuliwi rasmi hivyo katika Mataifa wanayofanyia kazi.

13. Vivyo hivyo, utambuzi wa Jamii Asilia katika mifumo ya kisheria ya ndani ni muhimu lakini mara nyingi hukosekana. Ushauri huko Asia ulionyesha kwamba wanapoainishwa kama "walio wachache", Jamii Asilia hujitahidi kudai haki zao na kutafuta haki kwa masuala kama vile kutoweka kwa lazima. Ukosefu huu wa utambuzi husababisha kutengwa kutoka michakato ya mashauriano na kupuuzwa kwa athari za uwekezaji wa kigeni na miradi ya maendeleo kwa ardhi zao, utamaduni, na lugha.

14. Watetezi wa Kizazi cha walio na asili ya Kiafrika (Afro-descendants) pia hawapati utambuzi wa kutosha. Mara nyingi huwekwa katika makundi ya Jamii Asilia au Jamii za walio wachache, licha ya kukabiliwa na hatari kubwa na zilizo wazi; jambo linaloangazia uhitaji wa rekodi sahihi, zaidi za data mahususi, kwa muktadha na mifumo ya ulinzi iliyoundwa. Jamii ya waGarífuna, katika Triunfo de la Cruz, huko Honduras, zinaonyesha mapambano yanayowakabili Jamii za Kizazi cha walio na Asili ya Kiafrika (Afro-descendants)[36] ambazo zimepitia unyang'anyi wa ardhi, huku sehemu za eneo lao la mababu zikiuzwa au kutengwa kwa ajili ya maendeleo ya utalii bila idhini yao. Mnamo 2020, watetezi watano wa ardhi wa Garífuna walichukuliwa kwa nguvu kutoka majumbani mwao na kutoweshwa kwa lazima.[37]

15. Jopokazi linasikitika sana kuona kuongezeka kwa uhalifu wa watetezi wa LNRE. Nchini Guatemala, kiongozi wa chama cha wavuvi kinacholinda vyanzo vya maji kutokana na uchafuzi wa mazingira alitoweka kwa lazima na baadaye akashtakiwa kwa madai ya unyang'anyi wa ardhi.[38] Vile vile, Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wa jamii za kiasili anasema kwamba watetezi wa LNRE mara nyingi hukamatwa kwa msingi wa "viwango duni vya ushahidi", "ushuhuda wa mashahidi usiothibitishwa", na bila "uhusiano wazi kati ya mashtaka na vitendo vinavyodaiwa".[39]

16. Kutambuliwa kama watetezi wa LNRE kunaweza pia kusaidia kupambana na uhalifu, unyanyapaa, utambuliso hasi na unyanyasaji. Wale wanaopinga uwekezaji wa kigeni, shughuli za uchimbaji madini, au miradi ya maendeleo mara nyingi huitwa na Mataifa au vyombo vya habari "wapinga maendeleo", "magaidi", au "magaidi wa mazingira". Mbinu hii inaripotiwa kutumika kulinda maslahi ya Serikali na makampuni, kudharau kazi ya watetezi, kuhalalisha ufuatiliaji, na kuwaunganisha na uchunguzi wa ugaidi[40], na kuongeza kwa kiasi

[35] Front Line Defenders, "Global Analysis 2023/24", 2024, p. 11-12. 2024. Kati ya ukiukwaji 1,538, ulioripotiwa zaidi duniani kote ulikuwa kukamatwa/kuzuiliwa kiholela (15%), hatua za kisheria (13%), vitisho vya kifo (10.2%), ufuatiliaji (9.8%), na mashambulizi ya kimwili (8.5%). Katika ngazi ya kikanda, ukiukwaji katika muktadha wa ulinzi wa LNRE ulitokea zaidi barani Afrika na Amerika.

[36] Jumuiya ya Triunfo de la Cruz ni sehemu ya the Black Fraternal Organization of Honduras (*Organización Fraternal Negra Hondureña*, OFRANEH), shirika linalofanya kazi kulinda haki za kiuchumi, kijamii, na kitamaduni za jamii ya Garífuna, ambao ni kizazi cha walio na asili ya Kiafrika..

[37] HND 2/2022, HND 3/2022, HND 2/2024 Tume ya Haki za Binadamu ya Amerika (IACHR) ishatoa hatua za tahadhari katika kesi hii.

[38] Tukio hilo liliripotiwa kama kizuizi cha kiholela na si kutoweka kwa lazima na UDEFEGUA"Informe 2018", p. 186.

[39] A/HRC/39/17, para. 49.

[40] Tume ya Haki za Kibinadamu ya Amerika. "Report on the Criminalization of the Work of Human Rights Defenders", paras. 57 na 63−71; Pia A/HRC/39/17, para. 32.

kikubwa hatari yao ya kutoweka kwa lazima. Nchini Ufilipino, kwa mfano, Jopokazi linabainisha kile kinachoitwa mazoezi ya "kuweka alama nyekundu", ambayo inadaiwa imetumika kuwalenga watetezi wa LNRE kwa kuwalinganisha kimakosa na wachokozi, na kusababisha kutoweka kwao kwa lazima.[41]

17. Kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE mara nyingi hutokea katika miktadha inayoundwa na ubaguzi wa kimfumo, vurugu za kimuundo, kasumba ya kikoloni, na ubaguzi wa kimazingira. [42] Inatumika kama zana ya ukandamizaji ili kuwanyamazisha watu waliotengwa, kuwanyima haki yao ya kusikilizwa katika michakato ya kufanya maamuzi, na kudhoofisha juhudi zao za kuunda mustakabali endelevu. Mojawapo ya viashiria vilivyo wazi kwamba Jamii Asilia kote ulimwenguni bado wanahitaji marekebisho ni ukosefu wao wa upatikanaji na usalama katika ardhi zao za kitamaduni.[43]

18. Jopokazi linaangazia kupotea kwa lazima kwa mwanaharakati wa mazingira Porlajee “Billy” Rakchongcharoen nchini Thailand, [44] mwaka 2014, jambo ambalo linaonyesha udhaifu na hatari kubwa zinazowakabili watetezi binafsi wa LNRE wakati kazi yao inawaleta katika mgogoro na watendaji wenye nguvu wa Serikali au kiuchumi. Bw. Rakchongcharoen, kiongozi wa Jamii Asilia ya wa Karen na mwanaharakati wa haki za ardhi, alikuwa akipanga kuishtaki Serikali na wanakijiji wengine wanaoishi katika Hifadhi ya Kitaifa ya Kaeng Krachan. Hii ilitokana na kuteuliwa kwa ardhi yao, bila mashauriano ya awali, kwa hatua za uhifadhi na juhudi za Serikali za kuwafurusha kwa fujo. Walipokuwa wakisafiri kukutana na wanakijiji, maafisa wa Hifadhi ya Kitaifa wanadaiwa kumkamata Bw. Rakchongcharoen, na kusababisha kutoweka kwake kwa lazima. Mkewe na binti yake wanatafuta kufafanua hatima yake na mahali alipo hadi leo.

19. Taarifa zilizopokelewa na Jopokazi pia zinaonyesha kwamba ukosefu wa michakato ya kutosha ya mashauriano katika upangaji wa miradi ambapo LNRE inaweza kuathiriwa ni sababu inayochangia kutoweka kwa lazima. Ukosefu wa mashauriano au mashauriano yenye dosari na jamii zilizoathiriwa mara nyingi husababisha uharibifu wa mazingira, kuhamishwa kwa lazima, na mapambano ya moja kwa moja na watetezi wa LNRE. Katika miktadha tofauti, mashauriano ya jamii[45] yasiyotozelesha, yenye dosari au yaliyopotoshwa huchochea migogoro na mvutano wa kijamii, na kuongeza hatari ya vurugu, ikiwa ni pamoja na kutoweka kwa lazima na mauaji. Mifumo rasmi ya mashauriano kwa wenyeji mara nyingi hupuuzwa, na mashauriano yanapotokea, kuna ripoti za ujumuishaji wa kupendelea au vitisho kwa washiriki, na, katika baadhi ya matukio, kutoweka kwa lazima.

20. Kushindwa kwa mataifa kugawa, kuweka mipaka, na kutoa hati miliki za ardhi kwa Jamii Asilia na jamii zingine, pamoja na kutochukua hatua za kushughulikia migogoro ya ardhi, pia ni sababu ya hatari ya kutoweka kwa watu kwa lazima, ambayo inaweza kuzidishwa wakati jamii hazina ufikiaji wa kutosha wa kilimo, au ulinzi wa utawala na raia wakati wa migogoro ya ardhi na makampuni ya biashara au Serikali. Kurekebisha umiliki wa ardhi na hati miliki kwa Jamii Asilia kunahusisha kupata haki zao za kisheria za ardhi, mara nyingi kulingana na umiliki na matumizi ya kitamaduni, na kutambua sheria na desturi zao za kitamaduni. Hii inalenga kuhakikisha upatikanaji wao endelevu wa rasilimali, riziki zao za kitamaduni, na uwezo wao wa kutawala maeneo wanayomiliki, huku pia ikizuia migogoro na kuhakikisha uhifadhi endelevu wa mazingira. Katika muktadha huu, Jopokazi limepitia kesi zinazoonyesha jinsi haki dhaifu za ardhi na mali na ukosefu wa idhini illiyoarifiwa na ya huru, unaviweka jamii katika hatari kubwa ya kutoweka kwa lazima.[46]

[41] PHL 1/2020; PHL 7/2019.Tazama pia uchunguzi wa awali wa Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu uhuru wa maoni na kujieleza, Bi Irene Khan,“Preliminary observations by the UN Special Rapporteur on freedom of opinion and expression, Ms Irene Khan, at the end of her visit to the Philippines”, 2 February 2024.

[42] A/HRC/48/78. Pia A/77/549, para. 16.

[43] FRA 5/2025.

[44] A/HRC/WGEID/132/1, para. 114.

[45] Kwa mfano, A/68/262, para. 51; A/72/170, para. 23; A/HRC/39/17, para. 36; na A/HRC/39/62, paras. 46 – 62.

[46] UGA 4/2024, TZA 1/2024 na USA 10/2024. Pia A/HRC/39/17, para. 30.

21. Kulingana na mashauriano, shughuli za kiuchumi na vivutio vinayohusishwa na mpito wa nishati na hatua za hali ya hewa, haswa kwa nchi zinazoendelea kiuchumi na ambazo hazijaendelea sana, kama vile miradi mikubwa ya nishati mbadala na kuongezeka kwa soko la kaboni la hiari,[47] husababisha hatari inayoibuka ya kutoweka kwa lazima. Mahitaji ya maeneo makubwa ya ardhi ili kusaidia miradi ya kukabiliana na kaboni kama vile upandaji miti, upandaji miti upya, na mipango ya uhifadhi yameongezeka sana. Ingawa mipango hii imeandaliwa kama suluhisho la hali ya hewa, inaweza kuchochea ununuzi wa ardhi unaopita au kupuuza haki za jamii zenye uhusiano wa kitamaduni au wa mababu na ardhi, na kusababisha mvutano ambao unaweza kuzidisha vurugu na kutoweka kwa lazima, kama ilivyojitokeza kutoka kwa mashauriano.

B. Muktadha wa kijiografia

22. Kila nchi na eneo huwasilisha wasifu tofauti wa hatari unaotokana na mchanganyiko wa mambo, ikiwa ni pamoja na taasisi dhaifu za serikali, ufisadi, uhalifu uliopangwa, migogoro ya silaha, na uwepo wa vikundi vyenye silaha visivyo vya Serikali, uwekezaji mkubwa wa kigeni, rasilimali nyingi za asili, na miradi mikubwa ya nishati.

23. Miradi ya uwekezaji wa kigeni, uchimbaji na maendeleo inayoathiri LNRE mara nyingi hupatikana katika maeneo ya vijijini yenye uwepo dhaifu wa Serikali, unaokaliwa na jamii ambazo hazijawakilishwa kikamilifu au zilizobaguliwa kihistoria. Kwa hivyo, watetezi wa LNRE hawako tu katika hatari ya kutoweka kwa lazima kutokana na uwepo wao ambapo ukiukwaji unafanyika, lakini pia kwa sababu wanapaza sauti zao kupinga. Kutokana na umbali wa maeneo mengi kati ya haya, watetezi wa LNRE hawawezi kutegemea mamlaka ya Serikali kwa ajili ya ulinzi. Ukosefu wa uwepo wa Serikali unamaanisha kwamba kutoweka kwa lazima mara nyingi hakuripotiwi na hakuchunguzwi. Katika miktadha kama hiyo, kutochukua hatua kwa Serikali kunaweza kumaanisha kukubali vitendo vinavyofanywa na wahusika wengine.

24. Ingawa utoaji taarifa zisizotosheleza bado ni wasiwasi katika maeneo mbalimbali, Jopokazi lilipokea taarifa za kutisha hasa kuhusu México, Honduras, Ecuador, Perú, Guatemala, Colombia na Brazil—zilizotambuliwa kama nchi hatari zaidi kwa watetezi wa LNRE huko Amerika Latini.[48] Colombia inasalia kuwa nchi hatari zaidi, ikiwa na idadi kubwa ya mauaji yanayohusiana na ulinzi wa ardhi.[49] Brazil inakabiliwa na changamoto za shughuli haramu na masuala ya usambazaji wa ardhi, ambayo yanachangia kutoweka kwa lazima.[50] Kutokujali kuendelea kwa kutoweka kwa lazima nchini Mexico, pamoja na madai ya kuhusika kwa uhalifu uliopangwa na kuongezeka kwa vurugu dhidi ya watetezi, ni jambo la kutia wasiwasi sana, pamoja na vurugu dhidi ya Jamii Asilia wanaotetea LNRE[51]. Nchini Nicaragua na Brazil, kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE kunadaiwa kuhusishwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa usawa katika usambazaji wa ardhi na shughuli haramu kama vile ukataji miti haramu.[52] Nchini Nicaragua, haswa, Jamii Asilia na wakulima wameathiriwa sana na kutoweka kwa lazima wakati wa kujaribu kutetea LNRE.[53]

25. Barani Afrika, kutetea LNRE ni hatari sana katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Ghana, Kenya, Nigeria, Tanzania na Uganda.[54] Madai ya kutoweka katika nchi hizi mara nyingi huhusishwa na maandamano ya kupinga unyonyaji wa ardhi na rasilimali. Hali nchini DRC inatia wasiwasi hasa, huku kukiwa na ripoti kwamba walinzi wengi wa

[47] Soko la kaboni la hiari (VCM) ni soko lililogatuliwa ambapo watu binafsi, makampuni, na mashirika wanaweza kununua na kuuza mikopo ya kaboni ili kukabiliana na uzalishaji wao wa gesi chafu. Mikopo hii inawakilisha miradi inayopunguza au kuondoa kaboni kutoka angani.

[48] Front Line Defenders, "Global Analysis 2023/24", 2024, p. 50 na A/HRC/46/35, para. 44.

[49] Ibid.

[50] Observatorio de la Desaparición de Personas en Brasil Informe de Brasil.

[51] Amnesty International. Mexico: Land and Freedom? Criminalization of Defenders of the Land, Territory and Environment.

[52] Ibid.

[53] Movimiento Campesino Nicaragua.

[54] Africa Network for Environment and Economic Justice. Pia Elizka Relief Foundation.

mazingira wameuawa, na hakuna uchunguzi sahihi uliofanywa ili kubaini kama pia walikuwa waathiriwa wa kutoweka kwa lazima.[55] Nchini Uganda, upinzani dhidi ya miradi kama East African Crude Oil Pipeline umeripotiwa kusababisha kukamatwa kiholela na kutoweka.[56] Nchini Nigeria, watu wa Ogoni wameripotiwa kuteseka kwa muda mrefu kutokana na uharibifu wa mazingira na ukandamizaji kutokana na unyonyaji wa mafuta.[57]

26. Barani Asia, kutokana na taarifa zilizopokelewa, nchi zilizoripotiwa kuwa hatari zaidi kwa watetezi wa LNRE ni Indonesia, Pakistani, Ufilipino, na Thailand.[58] Katika nchi hizi, kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE kunaripotiwa kuhusishwa na umiliki wa ardhi ya mababu, unyonyaji wa maliasili, ujeshi, na migogoro ya mazingira. Kwa mfano, desturi ya kutoweka kwa lazima imeripotiwa kutumika kama zana ya kukandamiza upinzani huko Balochistan, hasa kuanzia miaka ya 1970[59], huku ongezeko kubwa likitokana na Ukanda wa Kiuchumi wa China-Pakistan na miradi mingine ya maendeleo.[60] Kulingana na mawasilisho yaliyopokelewa, eneo la Bastar, nchini India, ni kitovu cha kutoweka kwa lazima na ukiukwaji wa haki za binadamu kutokana na uchimbaji wa madini na ujeshi mkubwa. Jamii za Adivasi nchini India zinaripotiwa kukabiliwa na ukandamizaji mkubwa, huku watetezi wa LNRE mara nyingi wakikamatwa kwa kuzingiziwa mashtaka ya uwongo au kuuawa.[61]

C. Utofauti wa waathiriwa

27. Baadhi ya makundi ya watetezi wa LNRE wanakabiliwa na mkingamano wa vitisho ambavyo huongeza hatari yao ya kutoweka kwa lazima. Watu binafsi na jamii ambazo tayari ziko pembezoni mwa jamii, kutokana na umri, ulemavu, utambulisho wa kijinsia, rangi, kabila, au hali ya kijamii na kiuchumi, hupata udhaifu ulioongezeka na unaokingamana, katika uwezekano wa kutoweka na athari zake. Katika muktadha wa watetezi wa LNRE, madhara si ya mtu binafsi tu bali ya pamoja, kwani kutoweka kwa kiongozi wa jamii au mtetezi huvuruga miundo ya familia, mshikamano wa kijamii, na hisia ya kuwa pamoja ambayo mara nyingi huvuka mipaka.

28. Wakati watetezi wanawake wa LNRE wanapotoweka kwa lazima au wanapohusika katika utafutaji wa wapendwa wao waliotoweka, wanakabiliwa na mkingamano wa vitisho unaotokana na ubaguzi wa kimfumo, unyonyaji wa kiuchumi na kutengwa kisiasa.[62] Wanapoongoza juhudi za kutafuta jamaa waliotoweka, mara nyingi huchukua majukumu mapya katika jamii zao, wakipinga kanuni za jadi za kijinsia na kukabiliana na vikwazo vya kitaasisi, kitamaduni, na kisheria vinavyotokana na miundo ya mfumo dume na kasumba ya ukoloni. Mara nyingi hulengwa na aina maalum za vurugu za kijinsia, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji, vitisho vya kijinsia na kashfa inayotokana na chuki dhidi ya wanawake. Katika visa vingi, hawaadhibiwi tu kwa ajili ya utetezi wao wa LNRE, bali pia kwa kukiuka dhana potofu za mfumo dume.

29. Kutoweka kwa watetezi wa LNRE ambao ni wazee au viongozi, hasa pale Jamii Asilia wanapohusika, hugawanya jamii, hudhoofisha uongozi, na kuzidisha udhaifu wa kiuchumi na kimazingira. Wakati mtetezi wa LNRE ametoweka kwa lazima, jamii iliyoathiriwa hupoteza mlinzi muhimu aliye na mizizi kwa haki yao ya mazingira, urithi wao wa kitamaduni, njia zao za kujikimu, na, kwa upande wa Jamii Asilia, haki zao za kujitawala na

[55] Maat for Peace, Development and Human Rights.
[56] Ibid.
[57] Angalia *Social and Economic Rights Action Center (SERAC) and the Center for Economic and Social Rights (CESR) v. Nigeria*, Communication 155/96, African Commission on Human and Peoples' Rights, 27 October 2001, and *SERAP v.* Nigeria, Judgment No. ECW/CCJ/JUD/18/12, ECOWAS Community Court of Justice, 14 December 2012.
[58] Asian Forum for Human Rights and Development (FORUM-ASIA).
[59] AL PAK 1/2025.
[60] Baloch Yakjehti Committee.
[61] International Solidarity for Academic Freedom in India (InSAF India) et al., "Enforced Disappearances of Adivasi Indigenous Peoples Resisting Takeover of Their Ancestral Lands to Facilitate Mining in Bastar Division, Chattisgarh, India".
[62] A/HRC/WGEID/98/2.

uhifadhi na ulinzi wa mazingira.[63] Zaidi ya hayo, wakati watetezi wa LNRE wanapotoweka kwa lazima, makundi yenye mshikamano hujikuta yakivunjika kutokana na huzuni, hofu, na ukosefu wa mwelekeo wazi. Watetezi wa LNRE ambao ni viongozi wa jamii na wazee pia mara nyingi hujumuisha na kusambaza maarifa muhimu kwa usimamizi wa ardhi, utambulisho wa kitamaduni, na mshikamano wa vizazi mbalimbali. Kupotea kwao hudhoofisha uhusiano wa jamii na kunyima vizazi vichanga mwongozo, na kuongeza udhaifu wa mmomonyoko wa utamaduni na unyonyaji wa mazingira. Athari hizi mara nyingi huwa sababu za kuwahamasisha wahalifu. Kwa mfano, kutoweka kwa lazima kwa Bw. Sombath Somphone[64] huko Lao PDR mnamo 2012 kulieleweka sana kama jaribio la kudhoofisha harakati za mazingira na maendeleo mashinani.[65]

30. Kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE kunadhoofisha zaidi juhudi pana za kimataifa za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira. Watetezi hawa hutumika kama mifumo ya tahadhari ya mapema na wawasilishaji muhimu wa athari za mabadiliko ya hali ya hewa, hutambua vitendo visivyo endelevu, hupinga miradi ya uchimbaji madini yenye uharibifu, na hupendekeza njia mbadala zinazofaa, zinazotegemea ujuzi wa kienyeji na maarifa asilia na usimamizi unaotegemea wenyeji. Kutoweka huku kwa lazima kunawazuia wengine kuzungumza kuhusu dhuluma ya mazingira, kuvunjwa kwa mitandao ya uanaharakati wa jamii, na kudhoofisha nafasi muhimu za mjadala wa umma. Wakati ambapo jumuiya ya kimataifa lazima ikabiliane kwa dharura na majanga matatu ya mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa viumbe hai na uchafuzi wa mazingira,[66] kutoweka kwa wale wanaoongoza mapambano haya kunahatarisha maendeleo ya masuluhisho yenye usawa, yanayozingatia haki na uendelevu. Kwa maana hii, kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE sio tu kukiuka haki za watu waliotoweka na zile za familia zao, lakini pia kunazuia juhudi za pamoja za kulinda sayari.[67]

31. Kwa jamii nyingi, ikiwa ni pamoja na Jamii Asilia, ardhi na mazingira si rasilimali tu, bali ni kipengele muhimu cha utambulisho wa kitamaduni [68] —hakuna utengano au mgawanyiko kati ya ardhi na wanadamu. Zaidi ya kuwa rasilimali inayoweza kutumika, ardhi inachukuliwa kama nafasi takatifu, kiini cha utambulisho katika ngazi za mtu binafsi na za pamoja.[69] Jamii hizi ni sawa na "Mama Dunia" na "Mama Asili", na zina uelewa tofauti kuhusu nani anaweza kuchukuliwa kuwa mwathirika katika visa vya kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE. Katika muktadha huu, uharibifu wa mazingira unaohusishwa na kutoweka kwa lazima unaweza pia kuonekana kama shambulio dhidi ya asili yenyewe. Kwa mfano, nchini Colombia, Mamlaka Maalum ya Amani (JEP) ilitambua Mto Cauca kama mwathirika baada ya kutumika kama kaburi la pamoja na vikosi vya kijeshi vinavyofanya kazi kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali kati ya 2000 na 2004.[70] Utambuzi huu hauonyeshi tu uharibifu wa ikolojia wa mto lakini pia madhara ya kiroho na kitamaduni kwa jamii zinazouzunguka. Utambuzi huu unawezesha kushinda dhana za kisheria zilizorithiwa ambazo huchukulia asili kama kitu na rasilimali inayoweza kutumiwa. Kutambua asili kama mada ya haki pia kunamaanisha kuonyesha wazi jukumu lake la kimuundo katika usawa wa hali zinazofanya uwezekano wa kuishi kwa sayari uwezekane.[71]

32. Kwa mfano, utaratibu mzuri unaotambuliwa ni sheria ya Colombia ambayo inawatambua wazi Jamii Asilia na jamii zao kama waathiriwa, ikisema kwamba "kwa Jamii Asilia, eneo hilo ni mwathirika, ukizingatia mtazamo wao wa ulimwengu na uhusiano

[63] A/HRC/30/38/Add.5.
[64] LAO 3/2012, LAO 2/2013, LAO 1/2021
[65] OHCHR, "'Where is Sombath?' Family of disappeared Lao activist demands answers", 4 October 2024.
[66] UN High Commissioner for Human Rights, "'Well past the hour' for countries to align climate laws with human rights obligations, says High Commissioner", 28 May 2024.
[67] A/HRC/56/46
[68] IACtHR. Comunidad Indígena Yakye Axa Vs Paraguay, para. 135.
[69] IACtHR. Comunidad Indígena Maya Q'eqchi' Agua Caliente vs. Guatemala, para. 103.
[70] Mamlaka Maalum ya Amani (SJP), Auto No. 226 de 2023, Caso 05. Tazama pia Special Jurisdiction for Peace. Katika muktadha wa Kesi 05 ya JEP, mkingamano kati ya kutoweka kwa lazima na uharibifu wa mazingira yanashughulikiwa.
[71] IACtHR, Advisory Opinion OC-32/25 of 29 May 2025

maalum na wa pamoja unaowaunganisha na Mama Dunia. Licha ya hayo, itaeleweka kwamba wenye haki chini ya amri hii ni Jamii Asilia na jamii zao na wanachama wao binafsi."[72]

D. Madhara ya vizazi mbalimbali

33. Kutoweka kwa lazima husababisha madhara kati ya vizazi. Kiwewe na kutokuwa na uhakika kuhusu hatima na mahali walipo wapendwa wao huathiri familia na jamii kwa miaka mingi, na matokeo ya kisaikolojia, kitamaduni, na nyenzo ambayo mara chache hurekebishwa. Hili linaonekana hasa katika visa vinavyowahusisha watetezi wa LNRE, ambapo jamii hupoteza sio tu watu binafsi, bali pia upatikanaji na ulinzi wa ardhi na rasilimali ambazo watu hao walipigania na kutetea.

34. Madhara ya vizazi mbalimbali yanayosababishwa na kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LRNE huathiri watoto hasa kwa njia zifuatazo: (i) kutenganishwa kwa kitamaduni: watoto hupata kutenganishwa na urithi wao wa kitamaduni wanapopoteza uhusiano na desturi zao za kitamaduni na lugha, ambazo ni muhimu kwa kukuza utamaduni wao; (ii) kupoteza uhusiano na ardhi yao: kuhamishwa kwa kulazimishwa kunazuia uwezo wa watoto kudumisha uhusiano na utamaduni wao, lugha, elimu, na afya, na hivyo kuathiri uwezo wao wa kutekeleza haki zao na kushiriki katika desturi za kijamii; (iii) kukatizwa kwa uenezaji wa maarifa ya mababu: kuhamishwa huko kunavuruga upitishaji wa maarifa na hekima ya mababu kuhusu ardhi kwa vizazi vipya, na hivyo kuathiri mwendelezo wa kitamaduni; (iv) athari tofauti kwa watoto: watoto wanalazimishwa kuishi katika tamaduni za kigeni, na kusababisha upotevu wa utambulisho na kung'olewa kwa kitamaduni; (v) kiwewe cha kisaikolojia: athari za kisaikolojia za kuhamishwa ni za vizazi mbalimbali, zinaathiri wazao wa waathiriwa na kuzuia maendeleo yao kamili; (vi) ukatili wa kijinsia: wanawake na wasichana wanakabiliwa na vurugu kubwa kutokana na kuhamishwa, kukata uhusiano wao na ardhi na rasilimali, na kudhoofisha mipango yao ya maisha na ile ya jamii zao.[73]

E. Uwandaraia Uliopungua

35. Kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE si kwa bahati mbaya, na kuna uhusiano wa moja kwa moja na kazi wanayofanya. Jopokazi limeandika ripoti nyingi za watetezi wa LNRE waliotoweshwa kwa lazima ili kuwazuia kufanya kazi yao halali ya kutetea ardhi, maliasili na mazingira. Kutoweka kwa lazima hutumika kuunda athari ya kutisha kwa ushiriki wa umma. Ukweli kwamba watetezi wengi wa LNRE pia hutoka katika jamii zilizoshikamana unamaanisha kwamba kutoweka kwa mtetezi mmoja kunaweza kuwazuia wengine wengi.[74]

36. Ingawa kupungua kwa nafasi ya kiraia (uwandaraia) kunaweza kusihusishe kutoweka kwa lazima, Jopokazi limeona ongezeko la matukio kama haya katika muktadha ambapo uhuru wa kujieleza, kukusanyika na kujumuika unazidi kuwekewa vikwazo. Mifumo kama vile kuenea kwa sheria au sera zenye vikwazo kuhusu uhuru huu inaweza kutumika kama onyo la mapema la hatari ya kutoweka kwa lazima. Kwa mfano, mnamo 2022, IACHR ililaani kufutwa kwa hadhi ya kisheria ya mashirika 25 ya kiraia, ikiwa ni pamoja na vikundi vinavyotetea mabadiliko ya hali ya hewa na haki za walio na asili ya Kiafrika (Afro-Descendants) katika pwani ya Karibea. Kabla ya mwezi moja kuisha, kiongozi wa Jamii Asilia, Salomón López Smith alikuwa amepatikana amekufa akiwa na dalili za mateso baada

[72] Decreto Ley 4633 de 2011, Colombia, Kolombia, Kifungu cha 3 (tafsiri isiyo rasmi).

[73] CCPR/C/143/D/4023/2021-4032/2021 aya. 8.4. Kamati ya Haki za Kibinadamu iliangazia madhara kadhaa makubwa yaliyosababishwa na kuhamishwa kwa lazima kwa Wenyeji—ambapo watu kutoka jamii hizi waliuawa na kutoweka—ambayo yana athari za vizazi mbalimbali. Pia: IACtHR. Comunidad Indígena Maya Q'eqchi' Agua Caliente vs. Guatemala, paras. 198 na 199.

[74] Amnesty International. Mexico: Land and Freedom? Criminalization of Defenders of the Land, Territory and Environment p. 53.

ya kutoweka kwa lazima kwa siku saba.[75] Jopokazi pia lilipokea taarifa kuhusu kesi ya kiongozi na mlinzi wa Jamii Asilia la Miskitu Bw. Brooklyn Rivera Bryan, pia huko Nicaragua, ambaye inasemekana alikamatwa kiholela mnamo Septemba 2023 na kutoweka kwa lazima.[76] IACHR ilitoa hatua za tahadhari kulinda maisha ya Bw. Rivera Bryan huko Nicaragua.[77] Hata hivyo hatima yake na mahali alipo bado haijulikani.

37. Jopokazi limerekodi visa kadhaa ambapo utumiaji wa uhuru wao wa kujieleza kwa watetezi wa LNRE umesababisha kutoweka kwa lazima au kuongeza hatari yake kwa kiasi kikubwa.[78] Kwa mfano, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao, watu huripoti hatari kubwa na hofu wanapotaja jina la mtetezi wa LNRE aliyetoweka, Bw. Sombath Somphone[79] (aliyetajwa hapo awali) kutokana na hofu ya kulipiza kisasi. Jopokazi pia lilirekodi kesi ya mkimbizi na mtetezi wa mazingira Bw. Od Sayavong, ambaye inasemekana alitoweshwa kwa lazima kutoka nyumbani kwake nchini Thailand kwa kulipiza kisasi mkutano wake na Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu umaskini uliokithiri na haki za binadamu.[80]

38. Watetezi wa LNRE pia wanakabiliwa na unyanyasaji wa kimahakama kwa kazi yao. Kwa kuzingatia ukosefu wa usawa wa rasilimali kati ya watetezi wa LNRE na mashirika ya kimataifa na makampuni mengine ya biashara, kwa mfano, katika suala la upatikanaji wa uwakilishi wa kisheria wa kutosha na unaofaa, hii inatoa changamoto kubwa. Watendaji wa serikali pia wamewalenga watetezi wa LNRE wanaotafuta taarifa kuhusu miradi ya maendeleo, wakiendesha kesi za kimkakati dhidi ya ushiriki wa umma (SLAPPs) ili kuwachosha na kesi za gharama kubwa na za muda mrefu[81]. Kwa mfano, kati ya 1997 na Mei 2019, mashirika nchini Thailand yamerekodi kesi 212 za SLAPP, huku 196 zikiwa kesi za jinai.[82] Mara tu wanapohusika katika vita hivyo vya kisheria, watetezi wa LNRE wanakuwa katika hatari zaidi ya kulipizwa kisasi kali, ikiwa ni pamoja na kutoweka kwa lazima, kutokana na kudharauliwa kwa jina na kazi zao, na hadhi yao iliyoongezeka kwa umma, miongoni mwa sababu zingine.

III. Walio na Hatia

A. Watendaji wa Serikali

39. Mataifa yana jukumu la msingi la kuzuia na kurekebisha ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na kushughulikia sababu kuu za kutoweka kwa lazima. Chini ya sheria ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Azimio la Ulinzi wa Watu Wote dhidi ya Kutoweka kwa Kulazimishwa na Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Watu Wote dhidi ya Kutoweka kwa Kulazimishwa, jukumu la serikali linaweza kutokea, sio tu kutokana na ushiriki wa moja kwa moja katika kutoweka, lakini pia kutokana na usaidizi, wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, ridhaa au kukubalia visa vya kutoweka vilivyofanywa na watendaji wasio wa Serikali.[83]

[75] Comisión Interamericana de Derechos Humanos, "Cierre del espacio cívico en Nicaragua", 2023.
[76] A/HRC/WGEID/132/1, para. 83(a) na A/HRC/57/54/Add.4, para. 32.
[77] Inter-American Commission on Human Rights, Resolution 59/2023, Precautionary Measure No. 799-23, 9 October 2023.
[78] THA 2/2016, IND 9/2019, AGO 1/2020.
[79] Supra note 51.
[80] THA8/2019, LAO 2/2019, THA 8/2020, LAO 4/2020, LAO 3/2023.
[81] OHCHR, "The impact of SLAPPs on human rights & how to respond", p. 2.
[82] Dialogue Earth, "In Thailand, SLAPP laws are silencing environmental journalists and activists", 28 November 2024, ikinukuu Human Rights Lawyers Association, "Overview of SLAPP cases collected from 1997 to 31 May 2019," Recommendations on the Protection of Those who Exercise Their Rights and Freedoms from Strategic Lawsuits Against Public Participations, p. 10.
[83] Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mkataba wa Kimataifa wa Kuwalinda Watu Wote dhidi ya Kutoweka kwa Kulazimishwa, 20 Desemba 2006, Kifungu cha 2 na Azimio la Utangulizi kuhusu Kuwalinda Watu Wote dhidi ya Kutoweka kwa Kulazimishwa.

40. Katika muktadha wa watetezi wa LNRE, ushiriki wa serikali katika kutoweka kwa lazima mara nyingi huchukua aina nyingi, zilizofungamana. Wajibu unaweza kutokea kupitia Serikali kuchukua au kutochukua hatua. Ingawa kutoweka kwa lazima mara nyingi huhusishwa na vikosi vya polisi au kijeshi, jukumu hilo pia linaenea kwa maafisa wa mitaa, ikiwa ni pamoja na mameya wa manispaa. Kutengwa kwa kihistoria kutoka kwa nguvu ya kisiasa kwa jamii zilizotengwa huunda miundo na mitazamo ya taasisi za Serikali leo, na kusababisha ubaguzi wa kimfumo, uhalifu, na kutojali vurugu dhidi ya jamii hizi—hali ambazo kutoweka kwa lazima kunawezeshwa, kuvumiliwa, au kupuuzwa.

41. Kwa upande wa watetezi wa LNRE, kutoweka kwa lazima mara nyingi hutokana na muunganiko tata wa sera za Serikali, maslahi ya makampuni, ajenda za maendeleo ya kimataifa,[84] ufisadi, kutokujali, na mienendo ya kisiasa ya ndani na kitaifa. Vitendo hivi vilivyofungamana, iwe ni kupitia ushiriki wa moja kwa moja, uwezeshaji, au uzembe wa makusudi, lazima vyote vichunguzwe ili kuelewa kikamilifu na kushughulikia jukumu la Serikali.

B. Watendaji Wasio wa Serikali

42. Kama ilivyoelezwa, jukumu la kisheria la kimataifa la Nchi linaweza kuchochewa na idhini, usaidizi au kukubali kwake katika utekelezaji wa kutoweka kwa lazima na "watu au vikundi vya watu" isipokuwa mamlaka ya nchi.[85] Katika baadhi ya miktadha, mwingiliano kati ya watendaji wa serikali na wasio wa serikali katika utekelezaji wa kutoweka kwa lazima ni mgumu, na ni vigumu kubaini kiwango cha ushiriki wa kila mhusika.

43. Jopokazi limetambua aina mbalimbali za watendaji wasio wa serikali wanaohusika katika kutoweka kwa lazima au vitendo sawa na kutoweka kwa lazima, kwa watetezi wa LNRE. Hivi ni vikundi vya uhalifu vilivyopangwa, mashirika ya kimataifa na makampuni mengine ya biashara, vikundi vya mamluki, makampuni ya usalama binafsi, taasisi za fedha, vikundi visivyo vya Serikali vyenye silaha, wamiliki wa ardhi, walowezi, na wengineo.

1. Vikundi vya uhalifu

44. Vikundi vya uhalifu vinaweza kutekeleza kutoweka kwa lazima vikiwa vimekubaliwa, kuvumiliwa au kuungwa mkono na Serikali, ili kulinda shughuli zao haramu. Wanaweza pia kuajiriwa na mamlaka za Serikali au makampuni ya biashara kufanya hivyo, ili kuficha msururu wa uwajibikaji kati ya wale wanaoamuru kitendo hicho na wale wanaokitekeleza.

45. Vikundi vya uhalifu vinaweza kuwaona watetezi wa LNRE kama vikwazo kwa shughuli zao zenye faida. Katika baadhi ya matukio, vikundi vya uhalifu hufanya kazi kwa ushirikiano na makampuni ya biashara na maafisa wa Serikali wafisadi, wakiwemo maafisa wa kijeshi. Katika baadhi ya maeneo, uhalifu uliopangwa umechukua udhibiti wa moja kwa moja wa unyonyaji wa maliasili, kunyang'anya jamii maeneo na rasilimali zao, na kufanya kutoweka kwa lazima kwa ustamilihivu au ushirikiano wa Serikali. Mifano inaonekana kwa udhaifu wa Jamii Asilia ya Amazon huko Brazil na hatari ya vurugu wanazokabiliana nazo kutokana na shughuli za wakataji miti haramu wanaotengeneza mbao kutoka Amazon[86]. Mfano mwingine ni kesi ya watetezi wa LNRE ambao walitoweka kwa lazima nchini Colombia baada ya wahusika wenye silaha kujaribu kunyakua ardhi yao kwa matumizi haramu.[87]

[84] UNODC, “The Drugs Crime Nexus in the Amazon Basin: How a complex crime ecosystem is endangering the world’s largest rainforest and imperiling efforts to combat climate change. The Drugs Crime Nexus in the Amazon Basin: How a complex crime ecosystem is endangering the world’s largest rainforest and imperiling efforts to combat climate change”, November 2023, p. 3.

[85] UN General Assembly, International Convention for the Protection of All Persons from Enforced Disappearance, 20 December 2006, Article 2.

[86] AL BRA 15/2021.

[87] IACHR, Res. 111/2021, Precautionary Measure No. 1113-21.

46. Kulingana na taarifa zilizopokelewa, vikundi vya uhalifu vilivyopangwa huko Guerrero, Mexico, vina uhusiano na mamlaka za Serikali, ambazo hushirikiana nazo kutekeleza kupotea kwa watu binafsi wanaotetea ardhi na maliasili zao.[88] Kupotea kwa viongozi wawili wa kijamii, Bw. Abencio Caicedo na Bw. Edison Valencia García, wanachama wa *Proceso de Comunidades Negras Palenque Regional el Congal*, nchini Colombia, kulitokea wakati wa uvamizi wa biashara haramu ya dawa za kulevya na uchimbaji madini katika eneo hilo, bila hatua madhubuti za utafutaji na uchunguzi kutekelezwa.[89]

2. Makampuni ya Biashara

47. Jopokazi limeona mwelekeo unaoonyesha athari za makampuni ya biashara yenye shughuli za kimataifa kutoka nchi zilizoendelea kiuchumi katika kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE katika nchi zinazoendelea kiuchumi. Jopokazi lina wasiwasi kwamba gharama ya kibinadamu ya juhudi za makampuni kama hayo ya kuongeza faida, au kuongeza faida kwa wanahisa wao, inabebwa sana na watetezi wa LNRE na jamii za vijijini. Katika nchi nyingi, ukosefu wa mifumo ya kisheria ya kuwawajibisha watendaji wasio wa Serikali kwa kutoweka kwa lazima, ikiwa ni pamoja na makampuni ya biashara, kwa kufanya kazi kwa idhini, usaidizi au idhini ya Serikali, huacha pengo kubwa la ulinzi na kukuza kutokujali.

48. Jopokazi limeona kwamba mataifa mengi hayana sheria thabiti na za lazima za uchunguzi wa kina. Ingawa viwango vya kimataifa vya haki za binadamu vipo, kama vile UNGP,[90] juhudi kubwa zaidi zinahitajika kwa nchi kupatanisha sheria zao za ndani ili kuanzisha majukumu ya makampuni kuhusu haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na kuweka vikwazo kwa kutofuata sheria. Hata hivyo, Jopokazi linaona maendeleo chanya ya hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kupitishwa kwa viwango vipya vya kimataifa ili kuongeza uwajibikaji wa makampuni. Ikumbukwe kwamba, Maagizo ya Umoja wa Ulaya 2024/1760 kuhusu Ustahimilivu wa Makampuni, ambayo yalianza kutumika Julai 2024, yanazitaka makampuni ya biashara kutambua, kuzuia, kupunguza, na kushughulikia athari za haki za binadamu katika msururu mzima wa shughuli zao, ndani na nje ya Ulaya. Zaidi ya hayo, Jopokazi linabainisha mwelekeo chanya wa kujumuisha masharti ya haki za binadamu katika Mikataba ya Uwekezaji wa Nchi Mbili, na kuimarisha zaidi mifumo ya kimataifa ya uwajibikaji wa makampuni.

49. Kuwajibisha makampuni ya biashara kwa kutoweka kwa lazima kunaweza pia kusababisha matatizo makubwa ya kisheria, ikiwa ni pamoja na kutambuliwa kisheria kwa makampuni ya biashara kama chombo chenye haki, asili yao ya kimataifa, ukosefu wa usawa wa rasilimali katika kesi na uhusiano wao wa karibu na Serikali.

50. Jopokazi limerekodi matukio kadhaa ambapo makampuni ya biashara, kwa kukubaliwa, kuvumiliwa au kuungwa mkono na Serikali, yamedaiwa kutekeleza kutoweka kwa lazima kwa watetezi wa LNRE.[91] Bw. Ricardo Lagunes Gasca na Bw. Antonio Días Valencia huko Mexico wametoweka kwa lazima kutokana na utetezi wao halali dhidi ya shughuli za uchimbaji madini, huku mamlaka ikidaiwa kupuuza kuchunguza uharakati wao wa mazingira.[92]

---

[88] Centro de Derechos Humanos de la Montaña Tlachinollan “Desapariciones forzadas en el contexto de la defensa de la tierra, el medio ambiente y los recursos naturales: el caso del estado de Guerrero”, p. 2.

[89] Asociación para la Investigación y Acción Social Nomadesc. Pia: IACHR, Res. 111/121 Precautionary Measure No. 1113-21.

[90] Guiding Principles on Business and Human Rights: Implementing the United Nations “Protect, Respect and Remedy” Framework.

[91] Guiding Principles on Business and Human Rights: Implementing the United Nations “Protect, Respect and Remedy” Framework.

[92] LUX 1/2023, MEX 1/2023 na ARG 1/2023, na TZA 1/2024, GBA 4/2024 na USA 10/2024, na Global Rights Advocacy (GRA), International Human Rights Clinic de Seattle University, Global Exchange and Tsikini.

